**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA KUMBUKIZI YA HAYATI DKT. JOHN POMBE JOSEPH MAGUFULI, ALIYEKUWA RAIS WA AWAMU YA TANO WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**CHATO, GEITA**
**TAREHE 17 MACHI, 2022**

**Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Awamu ya Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;**

**Wahashamu Baba Maaskofu;**

**Mheshimiwa Sheikh Abubakar Zubeir Ally Mbwana, Mufti wa Tanzania**

**Mzee Philip Japhet Mangula, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Tanzania Bara;**

**Ndugu Daniel Chongolo, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi;**

**Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;**

**Mheshimiwa Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Geita;**
**Waheshimiwa Wabunge;**

**Mheshimiwa Mama Janet Magufuli, Familia, Ndugu na majirani wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli;**

**Viongozi mbalimbali wa Serikali mliopo;**

**Viongozi wote wa Dini mbalimbali mliopo;**

**Familia ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli;**

**Wageni wote;**

**Wananchi wa Chato na watanzania wote kwa ujumla;**

**Wawakilishi wa Vyombo vya Habari;**

**Mabibi na Mabwana.**

***TUMSIFU YESU KRISTO***

Napenda nianze salamu za Serikali kwa kuungana na wote walionitangulia, kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema na fadhili, kwa kutupatia uhai na afya njema na kutuwezesha kukusanyika hapa Chato,

kwa ajili ya kumbukizi ya mpendwa wetu na Kiongozi wetu Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa awamu ya tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye alifariki dunia tarehe kama ya leo, mwaka jana 2021.

Napenda kuchukua fursa hii kuwaletea salamu kutoka kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aliniagiza niwakilishe Serikali katika kumbukizi ya mwaka mmoja tangu Kiongozi wetu mzalendo, mchapakazi na kipenzi cha Watanzania wanyonge Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alipoitwa kutoka dunia hii. Mheshimiwa Rais amenituma niwahakikishie kuwa Serikali yake itaendelea kumuenzi Kiongozi wetu huyo aliyetangulia.

Vilevile, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Mama Janet Magufuli na familia nzima ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa heshima kubwa waliyotupatia kama Serikali na mimi binafsi na Viongozi wenzangu kwa kutualika kujumuika nanyi, katika kumbukizi ya mpendwa wetu. Asanteni sana! Hatutaacha kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwapa neema na nguvu/kuyapokea mapenzi yake.

***Waheshimiwa Viongozi, Familia, Mabibi na Mabwana;***

Baada ya salamu naomba kumshukuru tena Mwenyezi Mungu kwa ajili ya maisha ya Hayati Dkt. Magufuli na kumwezesha kulitumikia Taifa letu katika nafasi mbalimbali za uongozi na kuacha alama chanya katika maendeleo ya nchi yetu. Leo hii Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli hayupo hapa pamoja nasi lakini kazi alizozifanya zitaendelea kuishi na kuongea. Napenda nikiri kwamba, si kazi rahisi kumwelezea kiongozi aliyekuwa na mafanikio makubwa kama Hayati Dkt. Magufuli. Hivyo leo nimechagua mambo machache sana katika kuadhimisha kumbukizi hii:

> **Kwanza**, ninamkumbuka Hayati Dkt. Magufuli kwa jinsi alivyomtanguliza Mungu mbele katika uongozi wake. Watanzania ni mashahidi jinsi ambavyo Hayati Dkt. Magufuli alivyotuongoza kumwamini Mungu na kumtanguliza katika kila jambo. Hata pale nchi yetu ilipopitia mambo magumu kama ukame, vimbunga na magonjwa hatari Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alitufundisha kutoogopa na badala yake alitutia moyo na kutusisitiza kuomba na kumtegemea Mungu. Alikuwa kiongozi mtendaji ambaye hakuishia tu kutoa maelekezo bali yeye mwenyewe alifunga na kuomba. Imani na ujasiri wake kwa Mungu ilituondolea hofu katika nyakati ngumu na za

hatari na kutuwezesha kupambana na changamoto tulizokuwa nazo. **Kwa hili, tutaendelea kumshukuru!**

**Pili**, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, anajulikana na kukumbukwa sana kwa falsafa yake ya ***"Hapa Kazi tu."*** Bila shaka utendaji wake wa kazi ulituvutia wengi na kutuhamasisha. Wengi wetu katika Serikali tulibadili mfumo wetu wa kufanya kazi ili kuendana na kasi yake. Nakumbuka nilipokuwa Waziri wa Fedha, ilikuwa ni kawaida sana yeye kunipigia simu usiku wa manane na kunipa maelekezo. Alitumia muda wake mwingi kuwafikiria watanzania hasa wanyonge na kuwafanyia kazi ili awaletee maendeleo kwa haraka. Kila mara Hayati alipenda kutukumbusha maandiko matakatifu kutoka Waraka wa pili wa Mtume Paulo kwa Wathesalonike (2 Wathesalonike 3:10) yanayosema *"Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili: kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula".* Hivyo, Watanzania hatuna budi kumuenzi kwa kuendelea kufanya kazi kwa weledi na bidii ya kiwango cha juu sana, iwe katika masomo, kazi za nyumbani, ofisini, kilimo, viwandani, biashara ama kutoa huduma kwa jamii na bila shaka katika utume wa kuhubiri neno la Mungu.

Kwa upande wa Viongozi tunajifunza kutoka kwa Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ujasiri na uthubutu wake katika kufanya maamuzi magumu kwa manufaa ya Taifa letu. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliamini kuwa ni bora kufanya maamuzi hata kama utakosea na ukajifunza kutokana na makosa hayo badala ya kutofanya maamuzi yoyote. Alichukizwa na viongozi waliokuwa hawafanyi maamuzi na kuchelewesha haki za wananchi au miradi ya maendeleo. Aidha, tunajifunza kutoka kwake umuhimu wa kuwajibika na kusimamia misingi ya haki na usawa katika kuwahudumia wananchi wote. Tunachota kwake umuhimu wa kupiga vita uzembe na rushwa kwa nguvu zote.

**Tatu,** Hayati Dkt. Magufuli aliamini kwa vitendo kuwa watanzania tunaweza kujiletea maendeleo yetu wenyewe. Hayati Dkt. Magufuli aliamini kuwa rasilimali za nchi yetu zikisimamiwa na kutumika vizuri zinaweza kututoa katika lindi la umasikini na kutuletea maendeleo. Sisi Watanzania ndio wenye wajibu wa kwanza kutatua matatizo ya nchi yetu na ya bara letu la Afrika, iwe ni matatizo ya kijamii, kisiasa au kiuchumi ili kukuza ustawi wa Taifa na bara zima. Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alisimamia mageuzi makubwa na magumu ya

kiuchumi na kujenga mifumo ya kisheria ya kusimamia rasilimali zetu hususan madini. Akijenga juu ya misingi ya Viongozi waliomtangulia chini ya uongozi wake madhubuti, uchumi wa Tanzania uliendelea kukua na kuimarika na tarehe 01 Julai 2020, Benki ya Dunia ilitangaza kuwa Tanzania imefikia uchumi wa kati wa chini yaani, *(lower middle income country).*

***Waheshimiwa Viongozi, Familia, Mabibi na Mabwana;***

Ni kutokana na kazi hizo, na nyingine nyingi, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, ataendelea kukumbukwa na kuwa katika vitabu vya historia ya Tanzania na Afrika. Hayati Dkt. Magufuli, ameingia kwenye orodha ya mashujaa na viongozi wetu mashuhuri ambao mchango wao katika nchi yetu kamwe hautasahaulika. Sisi kama watanzania tutaendelea kuenzi na kuthamini mchango wake katika maendeleo ya nchi kwa kufanya kazi bila kuchoka.

***Waheshimiwa Viongozi, Familia, Mabibi na Mabwana;***

Naomba nimalize salamu za Serikali kwa kuwashukuru wote waliofanikisha maandalizi ya kumbukizi hii, hususan familia ya Hayati Dkt. Magufuli, Kanisa, wananchi wa Chato, watu wote wenye mapenzi mema na wageni mlioweza kufika Chato, kushiriki shughuli hii muhimu ya leo kwa familia na Taifa letu la Tanzania. Najua kwamba Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kama binadamu mwingine yeyote alikuwa na mapungufu. Nawasihi sana wale wanaoendelea kuandika mambo yasiyostahili juu yake hasa kwenye mitandao ya kijamii waache. Mambo hayo yanaiumiza sana familia ya Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na ni kinyume cha mila na desturi za kitanzania. Watu hao watambue kwamba kila mmoja wetu siku moja atakufa. Tena, yeye asiyesamehe naye hatasamehewa (…….. quote bible). Nawasihi tuendelee kumwombea mpendwa wetu.

Raha ya milele umpe Ee Bwana, na mwanga wa milele umwangazie. Apumzike kwa Amani, Amina x 2. Raha ya milele uwape Ee Bwana na mwanga wa milele uwaangazie wapumzike kwa Amani. Amina.
Mwenyezi Mungu awabariki sana! Tumsifu Yesu Kristo!

**Asanteni kwa kunisikiliza.**